102/3

KISWAHILI

Karatasi 3

Februari/Mechi 2014

Muda: Saa 2½

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA MWIGO MDOGO 2014**

**FASIHI**

**Karatasi 3**

**Jibu maswali MANNE pekee.**

**Swali la kwanza ni la LAZIMA. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu NNE zilizosalia yaani, HADITHI FUPI, TAMTHILIA, USHAIRI na FASIHI SIMULIZI.**

**Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.**

**Kila swali lijibiwe katika karatasi tofauti.**

## SEHEMU A: RIWAYA

### KIDAGAA KIMEMWOZEA – Ken. Walibora

1. "Lakini *one day* muwapo wadosi msinisahau mwenzenu. *Promise* mazee hamtanisahau, jo.

a) Eleza muktadha wa usemi huu. {alama 5}

b) Taja mbinu moja ya uandishi iliyotumiwa katika dondoo hili. {alama 1}

c) Baadhi ya wahusika katika riwaya hii wanaendeleza maudhui ya UTU. Fafanua kwa kutoa mifano yoyote SABA. {alama 14}

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU B: HADITHI FUPI

### DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

**Damu Nyeusi – Ken. Walibora**

2. "Vita kati ya weupe na weusi, rangi mbili zinazokinzana na kufarakana ........... kuhusu kudhalilishwa kwa mtu mweusi."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. {alama 4}

b) Kwa kutoa mifano MINANE, thibitisha kuwa mtu mweusi amedhalilishwa. {alama 16}

3. **Maeko – Mohamed Khelef Ghassany**

a) Jadili nafasi ya mwanamme kwa kutoa hoja zozote sita. {alama 12}

b) Mwanamke ni mwenye msimamo dhabiti. Thibitisha ukweli wa kauli hii. {alama 8}

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**MTAHIKI MEYA - Timothy M. Arege**

4. Anwani ya tamthilia, Mstahiki Meya inafaa hadithi yenyewe. Jadili. {alama 20}

5. . . . sauti ni sauti tu! Wasemao mchana, usiku watalala. Waache waseme. Kelele za chura in kilele tu.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. {alama 4}

b) Taja na ufafanue maudhui yo yote manne yanayojitokeza katika dondoo hilo. {alama 16}

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU C: USHAIRI

6.

Oa, kwamba u muozi, uzoeleo kuowa,
Oa, mato maolezi, na mboni ukikodowa,
Oa, maji maundazi, meupe kama maziwa,
Oa, sizi ndizi ndowa, asokuoa ni yupi?

Oa, ndiwe muolezi, uzoeleo kuoa,
Oa, sifumbe maozi, maninga uchiyavuwa,
Oa, uzaze uzazi kama ulivyozaliwa,
Oa, sizi ndizi ndowa, asokuoa ni yupi?

Oa, maji t'imbet'imbe mema ya mtu kuyoa,
Oa, maozi sifumbe nawe tafurahiwa,
Oa, uole wapambe wako uliopambiwa,
Oa! Sizi ndizi ndowa, asokuoa ni yupi?

Oa, maji ya kisima, yatengenywe na mvuwa,
Oa, ukijitazama, kioo ukichanguwa
Oa, mwanamke tama, mtukufu wa sitawa,

Oa! Sizi ndizi ndowa, asokuoni yupi?

Maswali

a) Eleza maana NNE tofauti za neno oa kama lilivyotumiwa katika shairi hili. [alama 2]

b) Taja bahari mbili katika shairi hili. [alama 2]

c) Eleza kwa kutolea mifano mbinu mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa na mtunzi. [alama 4]

d) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. [alama 4]

e) Mtunzi ana maana gani asemapo "uole wapambe wako uliopambiwa" [alama 2]

f) Eleza umbo la shairi hili. [alama 4]

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa: [alama 2]

i) Sifumbe maozi

ii) 'Oa maji ya kisima yatengenywe na mvuwa'

7. KISU MKONONI:

Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja,
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
Siwezi, kama gurudumu nitajiviringisha
Mtelemko mkali huu
Lini na wapi mwisho sijui

Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu ya dhambi

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Kisu! Maisha kafiri haya
Kama kutazama nyuma na mbele
Ni kufa moyo mzima!

Sasa kama Simba - Mtu shauri nimekata
Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili
Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa,
Kila mpigo wa moyo wangu
Huu mpigo muziki wa maisha

**E. Kezilahabi**

a) Hili ni shairi la aina gani? [alama 2]

b) Taja sifa mbili za shairi la aina hii. [alama 2]

c) Eleza toni ya shairi hili. [alama 2]

d) Eleza ujumbe wa mtunzi kwa kifupi [alama 2]

e) Kwa kutolea mifano taja tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika shairi hili. [alama 2]

f) Mhusika katika shairi hili ana matatizo gani? [alama 2]

g) Ni kwa namna gani mhusika katika shairi ananuia kutatua matatizo yake? [alama 4]

h) Mtunzi ana maana gani anaposema [alama 4]

i) Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

ii) Kama simba – mtu shauri nimekata

## SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

8. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali:**

Ewe mainga wa ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopiga foleni
Chakula cha msaada kupata
Turudishe vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita
Matusi ukitema
Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
Uhitaji wetu ukatutuma
Kuokota vihela uloturushia
Ukatununua, kura ukapata?
Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Mainga wa ndumi huna lolote safari hii

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Ubunge umekudondoka ukitazama

Wanyonge tumeamua

Kwingine kujaribu.

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Maswali

a) Huu ni wimbo wa aina gani? Eleza kwa nini. {alama 2}

b) Eleza mbinu za lugha zilizotumiwa katika utungo huu. {alama 4}

c) Tambua nafsineni katika utungo huu. {alama 2}

d) Fafanua toni ya utungo huu. {alama 2}

e) Fafanua umuhimu wa nyimbo za aina hii. {alama 10}